

WARAKA WA KUENZISHA KITENGO

Waraka wa Fedha (TREASURY CIRCULAR No. 08 of 2001) ndiyo uliwezesha Serikali kuanzisha kitengo hiki cha Ukaguzi wa Kiufundi wa Miradi ya Maendeleo.

Waraka huu ulisambazwa kwa Maafisa Masuhuli wote wa Serikali ya Muungano – Tanzania Bara.

Wizara, na Idara zote za Serikali

Waraka uliwataka Wizara, Washauri Waelekezi, Wakandarasi wote na Wadau wengine wanaofanya kazi za Serikali au zile za Wafadhili pamoja na programu zote za maendeleo kwa maendeleo ya Watanzania watote taarifa na ushirikiano kwa Kitengo hiki wakati kinatekeleza kazi zake kama zilivyoainishwa kwenye waraka husika.



Wakaguzi wa Serikali wakikagua barabara iliyojengwa chini ya viwango.

Kwa Nini kuwa na Kitengo Hiki?

Kilianzishwa pamoja na mambo mengine kuongeza uwajibikaji katika matumizi ya pesa za umma (**to enhance public financial accountability and value for Money spent by the government of the United Republic of Tanzania on public programmes**).

Kitengo kinaongeza nguvu na juhudi za Idara na vitengo vingine ambavyo tayari vipo na vinavyofanya kazi za ukaguzi ndani ya mfumo uliopo wa Serikali.

Kitengo kinaongeza nguvu na juhudi za ziada kwa kuangalia zaidi masuala ya Kiufundi kwenye miradi ya maendeleo.

Kuangalia utekelezaji wa kazi kufuatia kanuni na sheria za mikataba, kuangalia viwango kama vinalingana na thamani ya fedha inayolipwa, n.k.



Wakaguzi wa Serikali wakikagua vifaa vya afya vinavyotolewa kwenye hospitali ili kuboresha huduma

Kitengo kinaangalia nini haswa?

Kinaangalia sehemu muhimu za miradi na programu za maendeleo ili kuboresha miundombinu, huduma za kijamii na uwezo wa taasisi kama ifuatavyo:

- Project Design
- Project Appraisal
- Project procurement (Works, goods and Services)
- Project Construction
- Project Maintenance
- Project Inspection

- Project Deliverance (Monitoring and Evaluation)

Jinsi gani Kitengo kinapaswa kufanya Kazi zake?

Kukagua kwa kuona kwa Macho (physical site visit)

Kukagua kwa kupima na kulinganisha vipimo hivyo na vile vinavyokubalika kitaifa na kimataifa.

Kulinganisha utekelezaji wa kazi kwa kuzingatia viwango (design and codes of practice)

Matokeo ya ukaguzi yanasadia kutoa tahadhari mapema ili kuzuia uwezekano wa madhara kutokea kwenye Mradi husika.

Kitengo kinatoa taarifa zake kwa Katibu Mkuu Hazina kwa kutoa maelekezo ya kuondoa dosari au kasoro zilizojitokeza wakati wa ukaguzi kwa manufaa ya mwendelezo wa Mradi husika.

Nyenzo (Miongozo) kwa ajili ya Utendaji kazi

- Uadilifu wa watumishi wake
- Sheria ya Fedha (Finance Act),
- Sheria ya Manunuzi (Procurement Act)
- Kanuni za Fedha (Financial Regulations)
- Kanuni za Manunuzi (Procurement Regulations)
- Waraka mbali mbali za Fedha (Treasury Circular Letters)
- Waraka Mbalimbali ya Serikali (General Orders)
- Waraka Mbalimbali za watumishi (Staff Circulars)

- Waraka na Barua mbalimbali za Utumishi Serikalini (Civil Service Department Establishment Circular Letters, etc)
- Sheria, Kanuni, Taratibu nyingine za Maadili ya kazi, n.k.

FAIDA ZA KUWA NA KITENGO

Kwa kuwepo na kitengo hiko ndani ya Wizara ya Fedha na Uchumi ambacho kinawajibika moja kwa moja kwa Katibu Mkuu Hazina, kutasaidia yafuatayo:

- Kuhakikisha utoaji huduma bora kwa Umma kulingana na fedha iliyolipwa au inayodaiwa.
- Kusaidia Hazina kutekeleza wajibu wake kikamilifu kama Mhifadhi Mkuu (Principal Guardian) kwa Faida ya Taifa kuweka udhibiti wa Bajeti
- Kudhibiti matumizi ya fedha na kuongeza ufanisi wa utendaji kazi wakati wa kutekeleza miradi ya maendeleo,
- kutoa huduma kwa jamii

UKAGUZI UNAFANYWA KATIKA MAKUNDI YAFUATAYO:

- Majengo
- Barabara na Madaraja
- Miradi ya Maji
- Miradi ya Mabwawa /Malambo na Skimu za umwagiliaji.

Katika kufanya kazi za ukaguzi wa kiufundi wa miradi kuthibitisha thamani ya kazi zilizofanyika kulingana na

fedha zilizotumika / zilizolipwa.

Kutoa ushauri wa kiufundi katika utekelezaji wa miradi kwa ajili ya kuepusha athari za hasara za kiutendaji (advisory services for an early intervention).

Kutoa ushauri wa kiufundi wakati wa kuandaa miradi kwa kulinganisha njia zinazotumika na vifaa vinavyotumika kutekeleza miradi hiyo (application of value engineering principles for the effective implementation of projects).

Kupitia na kushauri masuala ya migogoro wakati wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo na jinsi ya kuepukana na migogoro hiyo.

Kumshauri Katibu Mkuu Hazina kuhusu gharama halisi za kutekeleza miradi ya maendeleo, matatizo na ufanisi wa miradi hiyo kwa ajili ya matumizi ya uboreshaji wa sera na mipango ya baadaye.

Kitengo kinafanya kazi nyingine kulingana na mahitaji ya Katibu Mkuu Hazina au Wadau wengine wanaohitaji huduma hii.

**IMEANDALIWA NA WIZARA YA FEDHA
KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI,
S.L.P 9111, DAR ES SALAAM - TANZANIA
SIMU: +255 (22) 2111174/ 6, 2121935
BARUA PEPE: ps@mof.go.tz
TOVUTI: www.mof.go.tz**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA FEDHA

KITENGO CHA UKAGUZI WA KIUFUNDI WA

MIRADI YA MAENDELEO